Mfano Wa Mtego Wa Samaki

na

Ellis P. Forsman

Mfano Wa Mtego Wa Samaki

na

Ellis P. Forsman

Octoba 14, 2011

Mfano Wa Mtego Wa Samaki

Mat. 13:47-50

Mat. 13:47-50, "*Tena ufalme wa mbinguni umefanana na juya, lililotupwa baharini likakusanya samaki wa kila namna; hata lilipojaa walilivuta pwani wakaketi wakakusanya walio wema vyomboni, bali walio wabaya wakatupwa. Ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia; malaika watatokea watawatenga waovu mbali na wenye haki, na kuwatupa katika tanuru ya moto; ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.*"

Tunaambiwa kwamba ufalme wa Munga, au kanisa, ni kama mtego uliorushwa baharini, na kunasa samaki wa kila aina.

- Bahari ni dunia.
- Mtego ni kanisa.
- Samaki walionaswa "wa kila aina" ni washirika wa kanisa.
- Samaki wazuri ni wale wana wa Mungu wa kweli wa kiroho.
- Samaki wabaya ni wale watu waovu waliomo ndani ya kanisa.
- Pwani inawakilisha mwisho wa nyakati.
- Uchambuzi wa samaki huwakilisha Hukumu katika siku ya mwisho.
- Kukusanywa katika vyombo huwakilisha wokovu wa wale walio kimungu.
- Vyombo huwakilisha mbingu.
- Kutupwa mbali kwa wale wabaya ni kutupwa kwa waovu jehanamu.

Hebu tuangalie baadhi ya samaki tunazoweza kunasa katika mitego, na somo ambalo tunaweza kulipata.

Aina za samaki…

Rangi ya dhahabu

Ni wazuri kuangalia.

Mat. 5:16, "*Vivyo hivyo nuru yenu na iangaze mbele ya watu, wapate kuyaona matendo yenu mema, wamtukuze Baba yenu aliye mbinguni.*"

Kazi ya Mkristo lazima ionekane katika ulimwengu, ili kwamba ulimwengu utambue jinsi Mungu anavyowataka wawe. Lengo sio kuleta utukufu kwetu sisi, bali tunatenda matendo haya katika hali ya kumpa Mungu utukufu, na sio sisi binafsi.

Kwa bahati mbaya, wengi wanajitukuza wenyewe.

Mat. 6:1-2, "*Angalieni msifanye wema wenu machoni pa watu kusudi mtazamwe na wao; kwa maana mkifanya kama hayo hampati thawabu kwa Baba yenu aliye mbinguni. Basi wewe utoapo sadaka usipige panda mbele yako kama wanafiki wafanyavyo katika masinagogi na njiani ili watukuzwe na watu.*"

Kutenda matendo ya Mungu mbele za watu sio tatizo (kama nuru yetu kuangaza katika dunia), lakini tunapojipatia sifa katika haya (tukipiga tarumbeta kuhusu mambo mema tuyafanyayo), basi Mungu hapati faida.

Aina ya Wakristo walio na rangi ya dhahabu kama samaki. Kuna aina mbili tofauti za urembo, au mvuto katika ulimwengu. Kwa mfano: Mwanamke amevaa katika mfumo ambao ulimwengu unamtazama, na ulimwengu unaweza kusema kuwa ni mrembo; lakini mwanamke aliyevaa kwa heshima anaweza kuvutia kwa sababu atakuwa anaonyesha kwa mavazi yake kuwa yeye ni Mkristo, na Mungu atapata sifa.

Kamongo

Anaishi sehemu zenye tope. Wanapatikana Afrika na Amerika ya Kusini kimsingi wanajizika wenye kwenye tope wakati wa majira ya kiangazi wakati madimbwi yanakauka. Wanakaa pasipo kuwa na maji hadi mvua itakapo nyesha. Samaki huyu anatabia chafu na sio samaki mzuri kumla.

- Rum. 6:19-21, "*Nasema kwa jinsi ya kibinadamu kwa sababu ya udhaifu wa miili yenu. Kwa kuwa kama mlivyovitoa viungo vyenu vitumiwe na uchafu na uasi mpate kuasi, vivyo hivyo sasa vitoeni viungo vyenu vitumiwe na haki mpate kutakaswa. Kwa maana mlipokuwa watumwa wa dhambi, mlikuwa huru mbali na haki. Ni faida gani basi mliopata siku zile kwa mambo hayo*

mnayoyatahayarikia sasa? Kwa maana mwisho wa mambo hayo ni mauti."

- Efe. 5:3-5, "*Lakini uasherati usitajwe kwenu kamwe, wala uchafu wo wote wa kutamani, kama iwastahilivyo watakatifu; wala aibu wala maneno ya upuuzi wala ubishi; hayo hayapendezi bali afadhali kushukuru. Maana neno hili mnalijua hakika ya kwamba hakuna mwasherati wala mchafu wala mwenye tamaa, ndiye mwabudu sanamu aliye na urithi katika ufalme wa Kristo na Mungu.*"

Wakati mwingine wanadamu wanajiingiza katika mambo machafu.

1 Thes. 5:22, "*Jitengeni na ubaya wa kila namna.*"

Usiwe kama kamongo. Jitenge na uchafu, na uwe safi.

Pweza

Macho yamemzunguka; haikosi kuona chochote.

Mkristo alie na macho kama ya pweza hajioni mwenyewe, isipokuwa anaangalia tu makosa ya wengine.

Mat. 7:3-5, "*Basi mbona wakitazama kibanzi kilicho ndani ya jicho la ndugu yako, na boriti iliyo ndani ya jicho lako mwenyewe huiangalii? Au utamwambiaje nduguyo, niache nikitoe kibanzi katika jicho lako; na kumbe mna boriti ndani ya jicho lako mwenyewe? Mnafiki wewe itoe kwanza ile boriti katika jicho lako mwenyewe; ndipo utakapoona vema kukitoa kile kibanzi katika jicho la ndugu yako.*"

Kristo hasemi kwamba hatupaswi kujaribu kuwasaidia ndugu yetu akiwa na kosa, bali tunapaswa kuchukua mtazamo mzuri dhidi yetu. Je tunatatizo linalofanana ambalo linapaswa kushughulikiwa kwanza?

Dagaa

Ni wadogo, lakini wazuri kwa chakula. Wanaishi katika sehemu yenye mwanga katika dimbwi au ziwa, na ni haraka kuhisi hatari na kukimbia.

Wakristo wanapaswa kuwa kama dagaa. Tunatakiwa kuishi katika mwanga wa Kristo. Tunafanya hivyo kwa kuishi kulingana na neno lake.

- Zab. 119:105, "*Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu.*"

- 1 Yoh. 1:7, "*Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu Mwana wake yatusafisha dhambi yote.*"

Tunapojifunza neno la Mungu, na kutembea katika nuru yake sisi pia tunaweza kuhisi hatari na kukimbia, kama dagaa.

1 Tim. 6:11, "*Bali wewe mtu wa Mungu uyakimbie mambo hayo; ukafuate haki, utauwa, imani, upendo, saburi, upole.*"

Mumi

Anateleza na ni vigumu kumshika.

Mumi anawakilisha mtu ambaye haeleweki katika kanisa, kama vile tukio lililofanywa na Yohana Marko.

Mdo. 15:37-40, "*Barnaba akaazimu kumchukua Yohana aliyeitwa Marko pamoja nao. Bali Paulo hakuona vyema kumchukua huyo aliyewaacha huko pamfilia, asiende nao kazini. Basi palitokea mashindano baina yao hata wakatengana. Barnaba akamchukua Yohana Marko akatweka kwenda Kipro. Lakini Paulo akamchagua Sila akaondoka akiombewa na wale ndugu apewe neema ya Bwana.*"

Yohana Marko aliacha kazi yake ya kumtumikia Mungu na kumhudumia Paulo katika safari yake, lakini baadaye aligundua alichokifanya na akabadilika. Yeye na Paulo badaye wakarekebishana na wakawa na uhusiano wa karibu, na Yohana Marko wakawa vifaa muhimu katika kanisa.

2 Tim. 4:10, "*Maana Dema aliniacha akiupenda ulimwengu huu wa sasa, akasafiri kwenda Thesalonike; Kreske amekwenda Galatia; Tito amekwenda Dalmatia.*"

Dema pia alimwacha Paulo kwa sababu alipenda ulimwengu sana. Hatuambiwi kwamba Dema alibadilika.

Je waweza kutegemea kazi uliyoianzisha kwa ajili ya Bwana?

Usiwe Mkristo anayefanana na mumi. Simama imara katika Injili na huduma kwa Kristo.

Sangara

Tabia zake ni kwamba huwa mdadisi. Mara nyingi huweka pua lake katika mambo ya samaki wenzake. Hii sio ubora mzuri kwa Mkristo. Sizungumzii kumrekebisha mtu aliye na makosa ambapo maandiko kwa uwazi inafundisha, bali nazungumzia mtu anayejiingia katika maswala ambayo hausiki. Kwa mfano, miaka mingi iliyopita Lynell na mimi

tulikuwa tunaasili mtoto wetu wa nne, baadhi ya washirika wa kanisa wakatuijia wakisema haifai sisi kuwa na zaidi ya watoto watatu. Kwa vile maandiko yamenyamaza kuhusiana na watoto ambao mtu anafaa kuwanao, ni wazi kwamba hili lilikuwa ni swala la watu kujiingiza katika mambo yaw engine.

- 1 Pet. 4:15, "*Maana mtu wa kwenu asiteswe kama mwuaji, au mwivi, au mtenda mabaya, au kama mtu ajishughulishaye na mambo ya watu wengine.*"
- 1 Thes. 4:11, "*Tena mjitahidi kutulia, na kutenda shughuli zenu, na kufanya kazi kwa mikono yenu wenyewe, kama tulivyowaagiza;*"

Labda Yakobo angeshawishiwa na watu hawa wanaotuambia tusiwe na watoto zaidi ya watatu; kusingekuwa na Yusufu; tukiendelea zaidi pia kusingekuwa na makabila kumi na mbili ya Waisraeli.

Hebu tusiwe kama sangara.

Vibora

Vibora ni sawa na kamba mti, isipokuwa anaishi katika maji masafi yam to. Nilipokuwa mdogo, nilikuwa navua samaki hawa kwenye mito iliyokuwa ikiteremkia shambani mwetu. Sifa ya kipekee ya vibora ni kwamba anakwenda kinyume nyume. Mkia wake unanyooka alafu ugeuka mbele na kuifanya kwenda kinyume nyume. Mara nyingi huangalia ilipokuwa, kuliko anapokwenda.

- Luka 9:62, "*Yesu akamwambia mtu aliyetia mkono wake kulima, kisha akaangalia nyuma, hafai kwa ufalme wa Mungu.*"
- Ebr. 10:38-39, "*Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; naye akisita sita, roho yangu haina furaha naye. Lakini sisi hatumo miongoni mwao wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu.*"

Vibora anapenda chini ya tope. Mkristo anayefanana na vibora mara nyingi hutamani kurudi katika dhambi zake za nyuma, na mara nyingi hurudi katika njia ya dhambi. Mtu huyu hawezi kuwa katika kikapu cha samaki kikipelekwa katika ufalme wa mbinguni.

Mkristo lazima asimame na aishindanie imani.

Ngerengere

Ngerengere ni samaki ya msingi niliyewahi kumnasa nilipokuwa mtoto. Mara nyingi yuko chonjo, ankuwa macho. Mvuvi akipiga kelele, au akisimama mahali ambapo ni peupe anapovua hawezi akawa na bahati ya kumnasa.

Efe. 5:6-17, "*Mtu asiwadanganye kwa maneno yasiyo na maana kwa kuwa kwa sababu ya hayo hasira ya Mungu huwajia wana wa uasi. Basi msishirikiane nao. Kwa maana zamani ninyi mlikuwa giza, bali sasa mmekuwa nuru katika Bwana; enendeni katika nuru, kwa kuwa tunda la nuru ni katika wema wote na haki na kweli; mkihakiki ni nini impendezayo Bwana. Wala msishirikiane na matendo yasiyozaa ya giza, bali myakemee; kwa kuwa yanayotendeka kwao kwa siri, ni aibu hata kuyanena. Lakini yote yaliyokemewa hudhihirishwa na nuru maana kila kilichodhihirika ni nuru. Hivyo husema, amka wewe usinziaye, ufufuke katika wafu, na Kristo atakuangaza. Basi angalieni sana mnavyoenenda; si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima; mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu. Kwa sababu hiyo msiwe wajinga, bali mfahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana.*"

Wakristo wanatakiwa kuwa kama ngerengere: ambaye ni mgumu kudanganywa. Kutimiza hii, Wakristo lazima wafahamu kikamilifu mapenzi ya Mungu, na uongo wa ibilisi.

Kambale

Kambale hana mifupa; ni mlaini na hana umbo linaloeleweka. Anakwenda huku na huko, popote ambapo mawimbi huipeleka.

- Efe. 4:14, "*Ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja,, tukizifuata njia za udanganyifu.*"
- 1 Kor. 11:30, "*Kwa sababu hiyo wako wengi kwenu walio hawawezi na dhaifu na watu kadha wa kadha wamelala.*"

Tunapaswa kuwa na nguvu katika Bwana na uwezo wa ukuu wake, na tusiwe dhaifu kama kambale.

Efe. 6:10-18, "*Hatimaye mzidi kuwa hodari katika Bwanana katika uweza wa nguvu zake. Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzishinda hila za shetani. Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho. Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku*

ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote kusimama. Basi simameni hali mmejifunga kweli viunoni, na kuvaa dirii ya haki kifuani, na kufungiwa miguu utayari tuapatao kwa Injili ya amani; zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu. Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu; kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho, mkikesha kwa jambo hilo na kudumu katika kuwaombea watakatifu wote."

Hebu tusiwe Wakristo walio kama kambale.

Samaki Umeme

Anapatikana katka mto Ubelgiji Kongo. Ukimkamata anatoa mshituo uliosawa na beteri ya wait sita.

Baadhi ya waumini wa kanisa ni wa jinsi hiyo: hulewa. Kwa sababu moja, au nyingine, ni wachungu na wanahasira juu ya kitu fulani, na unaadhiri uhusiano wao na wengine na majukumu yao kwa Kristo.

Efe. 4:31-32, "*Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya; tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi.*"

Kama wewe ni Mkristo aliye kama Samaki Umeme, weka mbali hasira yako, na uweke upendo wa Kristo katika maisha yako.

Besi ya blu

Ni chakula kizuri; anaishi kwenye miamba na sio kwenye tope na sehemu safi.

- Mat. 7:24-25, "*Basi kila asikiaye hayo maneno yangu na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba.*"
- 1 Kor. 15:58, "*Basi ndugu zangu wapendwa, mwimarike, msitikisike, mkazidi sana kutenda kazi ya Bwana sikuzote, kwa kuwa mwajua kwamba taabu yenu siyo bure katika Bwana.*"

Mristo aliye besi ya blu na akipatikana juu ya mwamba, Yesu Kristo na mara nyingi ukae katika kazi yenu kwa ajili yake.

Hitimisho

Yote hayo hapo juu yaweza kupatikana katika kanisa la Bwana wetu, lakini wale wasio panda watakusanywa nje:

- Baadhi ya samaki wa dhahabu – hebu matendo yetu yaonekane na watu.
- Pweza: anahisi hatari kwa haraka na kukimbia.
- Kambale: yuko chonjo, yuko macho, na ni vigumu kumdanganya.
- Besi ya blu: anaishi maisha masafi, na yuko katika msingi imara.

Tukiishi ivyo, wakati hatima ya mwanadamu utakapofika, tutasikia.

Mat. 25:34, "*Kisha mfalme atawaambia wale walioko mkono wake wa kuume, Njooni mliobarikiwa na Baba yangu, urithini ufalme mliowekewa tayari tangu kuumbwa ulimwengu;*"